

Uhuru 14-12-87

# Mwanamuziki ashutumu magaidi wa MNR

MAPUTO, Msumbiji

Bw. Bob Geldof, ambaye ni mwanamuziki mashuhuri wa kikundi cha Rock Star anayepiga muziki kuchangia watu wanaokabiliwa na njaa duniani amewashutumu magaidi wa MNR kwa kusababisha dhiki na njaa kwa

(Musician condemns  
MNR bandits)

mamilioni ya wananchi wa Msumbiji.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumamosi iliyopita mjini hapa Bw. Geldof alisema, "Magaidi wa MNR wanatumia chakula kama silaha ya vita."

"Nilishitushwa sana na hali ilivyo", alisema kwenye mahojiano na waandishi wa habari mwishoni mwa ziara ya siku nne nchini Msumbiji.

"Nilikuwa nafahamu chanzo cha hali hiyo lakini sikuwa nimejiweka tayari kuona maonevu na uvunjaji wa haki usiovumilika hivi sasa ndani ya nchi hii ambayo inasababishwa na wahuni hao wa MNR," alisitiza.

Mwanamuziki huyo ambaye ni raia wa Ireland na mlezi wa Shirika la Muziki kwa watu walifika na njaa, aliwasili Msumbiji akitokea Ethiopia.

"Asilimia 80 ya njaa nchini Ethiopia inatokana na ukame ambapo nchini Msumbiji asilimia 90 ya njaa inatokana na msukosuko wa kisiasa..."

Serikali ya Msumbiji imekwishaelsea za kuwa watu milioni 4.5 kati ya watu wapatao milioni 12, wanakabiliwa na njaa.

Bw. Geldof pia ameushutumu vikali utawala wa Makaburu wa Afrika Kusini kwa kuwaunga mkono magaidi wa MNR katika vita hivyo ambavyo vimedumu kwa zaidi ya miaka 11 sasa.

"Huna haja ya kuona bunduki inayofuka moshi wa risasi ili ujue kwamba Afrika Kusini inaunga mkono vita hiyo..." alisema.

Katika ziara yake nchini Msumbiji, Bw. Geldof alikutana na watoto ambaao waliwahi kutekwa na magaidi hao wa MNR na kulazimishwa kuunganá nayo katika vita hivyo lakini baadaye wakakombolewa na majeshi ya serikali ya Msumbiji.